JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0746499926/0682825963

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

KUMB.NA: ILLGSS/FV/2022/ **Tarehe : 31.03.2022**

MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KWA MWANAO**

……………………………………………………………………………………… KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO TAHASUSI YA …………. KATIKA SHULE YA SEKONDARI ILULU KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023.

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Ilulu kwa mwaka wa masomo 2022/2023

Nampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake, akumbuke kwamba hii ni bahati kubwa na ya pekee kwake.

Shule ya Sekondari Ilulu ipo Mkoa wa Lindi Wilaya ya Kilwa. Usafiri wa mabasi ya KILWA yanapatikana Mbagala Rangitatu, utashuka kijiji cha NJIANNE shule ipo mita 300 toka kituo cha basi. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………………/2022

Pamoja na barua hii, pokea,

(a) Fomu ya kupimwa afya ya mwanafunzi. Apimwe kwenye Hospitali ya Serikali, hakikisha anapimwa sio kujaziwa fomu tu, na umwelekeze Mganga/Daktari matatizo ya afya aliyonayo, kwani hatutapokea hoja zozote za ugonjwa kinyume na ripoti ya daktari.
(b) Fomu ya kuonyesha ndugu wa karibu, ikiwa na anuani, namba ya simu na mahali anakoishi. Pia fomu ya ahadi ya kutekeleza wajibu. Kwa kumalizia, nakutakia maandalizi mema na safari njema kuja kujiunga nasi. (MOTTO "ELIMU KWA MAENDELEO").

KARIBU ILULU SEKONDARI

---------------------------------
Amina S. Mandai
Mkuu wa shule

THE HEADMISTRESS
ILULU SEC. SCHOOL
P.O. Box 139
KILWA - MASOKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0746499926/0682825963

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

Mambo muhimu ya kuzingatia

Sare ya shule:

- Mwanafunzi aje na sketi mbili za damu ya mzee (maroon) kitambaa kizito. Sketi zake ziwe ndefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi zisizidi sentimita 18 au inchi $7^1/_2$. Zingatia vipimo.
- Sketi zake ziwe na (belt) mkanda, upana wa belt usizidi sentimeta 5 au inchi moja na nusu
- Mshono wa sketi ni linda box (Linda kubwa mbele na nyuma).
- Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sketi/shamba dress kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa, atarudishwa nyumbani ili aje na sare zilizoelekezwa
- Mwanafunzi anaweza kushona idadi ya sare kadri ya uwezo wake. Ila inashauriwa awe na angalau sare za darasani mbili na gauni za kazi mbili.

Sare ya shule ni kama ilivyoelekezwa katika maelekezo. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare wakati wote wa masomo, na anapokwenda hospitali, mjini au anapokuwa katika shughuli zozote za kishule nje ya eneo la shule. Ni marufuku kabisa kujipamba wakati amevaa sare ya shule akiwa shuleni. Aidha, lipo vazi la kazi za nje ambalo huvaliwa na wanafunzi wanapokuwa katika kazi za mikono nje ya masomo

Aidha mwanafunzi anapaswa kuwa na sare zifuatazo:-

(i) Shati (blauzi) nyeupe mbili (2) au zaidi mikono mifupi tetroni – Tomato
(ii) Soksi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi
(iii) Kwa wanafunzi wa Kiislamu:
  - Nusu kanzu
  - Hijabu ya tetroni nyeupe ya kitamba cha halua na sio mtandio, isiwe na urembo wowote. Pia isiwe na urembo wa lessi.

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu (kamba) (VISIWE NA VISIGINO VIREFU) jozi mbili.
(v) Jezi (bukta na t-shirt) nyeusi kwa ajili ya michezo
(vi) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo
(vii) Track Suit nyeusi isiyobana, isiyokuwa na maandishi na yenye mistari meupe kwa ajili ya maandalizi ya jioni.
(viii) Gauni la kazi za nje la kitambaa kizito (shamba dress) rangi ya blue ya bendera ya taifa mshono wa solo ya kuunga, kama anavaa hijabu ashone rangi ya blue.
(ix) Aje na T-shirt rangi ya njano yenye kola ya ufito mweusi na njano, utagongewa nembo kwa Tsh 4000/= AU aje na Tsh 13000/= atapata T-shirt yenye nembo ya shule
(x) Sweta rangi ya damu ya mzee lenye nembo ya shule kwa anayehitaji linapatikana shuleni kwa Tsh 14,000/= au uje na sweta lenye muundo wa V mbele na utagongewa nembo kwa Tsh 2000/=

**NB:** Fedha ya T- shirt na sweta iletwe mkononi (cash) isiingizwe bank

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

Mahitaji mengine muhimu kwa mwanafunzi

i. Aje na sanduku (sanduku la bati) linalofunga vizuri kwa kuhifadhia nguo na vitu vyake. ii. Aje na godoro 3x
   a. Aje na vifaa vya usafi binafsi kama mswaki, sabuni n.k iv. Aje na Mto na Foronya yake ya bluu bahari kwa
ii. anayetumia
iii. Shuka za kulalia jozi (pair) mbili za futi 3x6 (rangi ya bluu bahari isiwe na maua)
iv. Taulo moja(1) au mbili (2)
v. Kandambili kwa ajili ya kuogea.
vi. Viatu vya plastiki chipsi rangi yoyote - vya kushindia
vii. Ndoo ndogo mbili (matumizi yake binafsi bwenini)
viii. Alete container lenye mfuniko/ sahani, bakuli, kikombe na kijiko (vyombo vya chakula)
ix. daftari ( kaunta books) quire three kumi (10)
x. Mathematical set moja (1) kwa matumizi yake awapo darasani
xi. Vitabu vya ibada kwa mujbu wa dhehebu lake.
xii. Leta nakala halisi ya result slip ya kidato cha nne

xiii. Leta nakala (kopi)ya cheti cha kuzaliwa

xiv. Alete na neti nyeupe ya kitanda cha futi 3x6
xv. Dissecting kit (kwa wanaosoma Biology)
xvi. Koti la maabara jeupe (wote kwa wanaosoma sayansi)
xvii. Kwa wanafunzi watakaosoma BAM ni vizuri wanunue Scientific Calculator Graph pad moja (1) kwa wanaosoma geography na masomo ya sayansi
xviii. Kama una bima ya afya njoo nayo, kama huna njoo na pesa CASH Tsh 50400 kwa ajili ya bima ya afya ya NHIF utakayotumia popote Tanzania kwa muda wa mwaka mmoja

VIFAA VYA USAFI

i. Soft broom moja (fagio laini la ndani)
ii. Hard broom moja (fagio gumu la ndani)
iii. Drier moja (mopa)
iv. Dawa ya chooni lita 2. Au uje na Tsh 4,000/= utapata lita 2 shuleni
v. Pia aje na vifuatavyo kulingana na tahasusi yake kwa ajili ya usafi
   - HGL - Panga na Brashi ngumu yenye mpini mfupi wa mbao/mti moja kwa ajili ya kusafishia sinki la choo. Asilete yenye mpini wa plastic
   - HKL – Fyekeo na ufagio wa chelewa ya wima
   - 

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

. .

CBG & HGK - Jembe lenye mpini

NB: Mwanafunzi alete kifaa na sio pesa.

## MICHANGO MINGINE

i. Fedha kwa ajili ya Taaluma Tsh 20,000/= kwa mwaka
ii. UkarabatiTsh 15,000/= kwa mwaka
iii. Watumishi vibarua Tsh 30,000/= kwa mwaka (wapishi, ulinzi na watumishi wasioajiriwa na serikali)
iv. Fedha za kitambulisho na picha Tsh 6,000/=
v. Nembo ya shule 4,000/= kwa mashati 2

Ream mbili (02) za karatasi kwa mwaka, moja ya ''Photocopy A4'' na moja ya mistari

(rulled)

vi. Kila mwanafunzi atatoa Tsh 5,000/= za tahadhari, Fedha hizi hazitarudishwa amalizpo shule kwani zitasaidia kukarabati vifaa ambavyo atakuwa amevitumia miaka miwili (tear and wear)

NB: VIFAA VYOTE VYA USAFI, DARASANI, DAWA YA CHOONI NA GODORO VINAPATIKANA DUKA LA SHULE, MADUKA NA STATIONERY ZA KARIBU, UNAWEZA UKALETA AU UKAJA KUNUNUA HUKU.

Ada ya shule

Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh 70,000/= Unaweza kulipa nusu Tsh 35,000/= muhula wa kwanza na nusu nyingine Tsh 35,000/= muhula wa pili. Ada na michango yote itumwe kwenye akaunti ya shule NAMBA 70103200012 Benki ya NMB (Ilulu Secondary School – Development account) na mwanafunzi afike na risiti halisi (Original) ya Benki..

**Fedha za matumizi**

Mwanafunzi afunguliwe akaunti benki ya NMB / CRBD kwa ajili ya kumtumia na kutunza pesa za matumizi binafsi.

### Chakula

Shule hutoa chakula ambacho huliwa na watanzania wote ambacho serikali inapendekeza kuliwa na wanafunzi. Endapo ana miiko ya kutokula vyakula fulani, tafadhali usipokee nafasi hii kwani shule haitatoa huduma pekee kwa kila mwanafunzi. Pia shule haitoi kibali kwa mwanafunzi kujipikia hivyo asilete chakula kama mchele, unga, biskuti, mkate, kinywaji cha aina yoyote n.k na haturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula/ kinywaji toka nje ya shule.

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

Nguo nyingine

Aje na nguo za ndani pamoja na khanga au kitenge doti moja tu. Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule, mwanafunzi anaruhusiwa kuvaa Track Suit wakati wa maandalio ya jioni ili kujizuia na mbu. Kinyume na hapo atarudishwa nyumbani kurejesha nguo zisizotakiwa kwa gharama zake.

ANGALIZO KWA MZAZI

i. Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, hivyo inakuwa ni mihula mirefu miwili na mifupi miwili kwa mwaka. Mzazi/mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto anawasili kwa wakati shuleni, vinginevyo sheria itachukua mkondo wake.
ii. Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi. Mwanafunzi haru usiwi kuwa na simu ya mkononi awapo shuleni.
iii. Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.
iv. Mzazi/mlezi kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivu wa maisha ya shule na kuvunja sheria za shule.
v. Siku ya kuwatembelea wanafunzi ni jumamosi na jumapili ya mwisho wa mwezi tu, muda ni kuanzia saa nne asubuhi hadi saa kumi na moja jioni.
vi. Shule ina utaratibu wa kudhughulikia usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mbali kipindi shule inapofunga. Hivyo mzazi/mlezi utapewa taarifa kabla ya shule kufunga, ili utume nauli.
vii. Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo
viii. Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara, tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa muuguzi wa shule. Hii itarahisishia shule kumhudumia. Usipofanya hivyo shule itashindwa kumhudumia. Usifiche ugonjwa, utapokelewa tu, kupata elimu ni haki yake.
ix. Mwanafunzi anaruhusiwa kuleta pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo zake. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme ama kifaa chochote kinachotumia umeme. Akibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa shule.
x. Shule itakapofungwa, likizo zote mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi wake (nyumbani kwao) na shule itakapofungua atatokea nyumbani kwao (kwa mzazi/mlezi) moja kwa moja kuja shuleni. Atakayekiuka utaratibu huu atarudishwa nyumbani kwa gharama zake.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na kumiliki simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu, hata kama anatoka mbali. AKIJA NAVYO ATAFUKUZWA SHULE (ATAFUTWA MASOMO MARA MOJA)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

N.B: Tafadhari mshauri mwanao azingatie/afuate maelekezo yote aliyopewa! Akipatikana na kosa litakalimsababisha arudishwe nyumbani, atajigharamia nauli ya kwenda na kurudi.

Sheria za shule

(a) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote
(b) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wanafunzi wanzake, kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, jiko la shule n.k
(c) Yakupasa kuweka shule, eneo lake na wewe binafsi katika hali ya usafi wakati wote
(d) Mwanafunzi aheshimu kengele, awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa
(e) Mwanafunzi anapaswa kuwa kimya darasani wakati wa kujisomea.
(f) Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule au makamu wake
(g) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au viambatanisho vyake kama charger, line, earphones'' pamoja na redio
(h) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu popote bila kibali cha uongozi wa shule, ili kuepuka upelekaji wa taarifa zisizo sahihi kwa wazazi. Mawasiliano yote yatafanywa kupitia ofisi ya makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi tu.
(i) Wanafunzi hawaruhusiwi kuja au kuletewa chakula cha aina yoyote toka nyumbani
(j) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mazungumzo na ndugu/jamaa yake msikitini, kanisani au hospitalini. Kama ndugu/jamaa huyo ana maagizo afike ofisini aonane n uongozi wa shule
(k) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalum.
(l) Mafuta yenye harufu kali, perfume/spray, poda, rangi za kucha na midomo, wanja, curl,nywele za bandia, mapambo kama bangili, heleni, mikufu n.k. havitakiwa kabisa shuleni
(m) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa,Wimbo wa Taifa, Wimbo wa shule, wombo wa Tanzania Tanzania Nakupenda kwa Moyo Wote na Tazama Ramani (kila mwanafunzi anatakiwa ajue kuimba nyimbo hizi
(n) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi ai wakati wa kazi, (mwanafunzi mgonjwa anapaswa kupumzika katika zahanati za shule).
(o) Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa
(p) Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele, wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni, urefu unaowezesha kijiti cha kiberiti kuonekana. Haruhusiwi kunyoa kipara au mitindo mingine kama kiduku, kijoti, kiseven n.k
(q) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo shuleni
(r) Ni marufuku kumruhusu mgeni kufika katika eneo la mabwenini
(s) Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu ambaye si mwanajumuiya wa shule hii isipokuwa kwa kusalimia

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

(t) Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shule ndiye anaruhusiwa kumwombea ruhusa mwanafunzi kama kuna tatizo. Pia ndiye atakayekuja shuleni pindi atakapohitajika kufanya hivyo
(u) Wakati wa kufunga shule wanafunzi wote wataondoka kwa pamoja kwa usafiri utakaoratibiwa na shule. Hakuna ruhursa yoyote itakayotolewa mapema kabla ya siku rasmi ya kufunga shule
(v) Kama mwanafunzi atapatikana na kosa la kinidhamu, mzazi au mlezi ndiye atakayetakiwa kufika shuleni na si mtu mwingine yeyote kama babu, bibi, mjomba, shangazi, kaka n.k.
(w) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga au kupigana na mtu yeyote awapo shuleni
(x) Mwanafunzi haruhusiwe kutumia lugha chafu.
(y) Mwanafunzi haruhusiwi kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(z) Mwanafunzi haruhusiwi kuanzisha, kushawishi na kushiriki mgomo.
(aa) Mwanafunzi atakaye toka mazingira ya shule bila kibali/ruhusa ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA

Mwanafunzi atafukuzwa shule au kusimamishwa masomo kwa muda (suspension) iwapo atakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule:

NB: MWANAFUNZI HATOPOKELEWA IKIWA ATARIPOTI BILA KUJAZA FOMU ZILIZOAMBATANISHWA

## KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KWA MWAKA 2022

Mimi ………………………………………………………… nakutaarifu kuwa nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Ilulu. NIMEKUBALI/NIMEKATAA nafasi hii baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu na barua ya kujiunga.

Ninaahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nikishafika shuleni, nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule kwa kipindi chote cha mimi kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilulu. Na nimeelewa kanuni na taratibu zote za shule na sitajihusisha na vitendo vya uvunjaji wa amani shuleni, kushiriki kufanya fujo, vurugu, migomo, kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na makosa ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

Jina la mwanafunzi ………………………………… Saini ….….……...Tarehe ……….

Jina la Mzazi/Mlezi …………………………………Saini …………….Tarehe ……….

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

FOMU NAMBA 1.

To the Medical Officer
……………………………………………………………………….….
……………………………………………………………………….

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO …….…………………………………………

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school students.

1. Blood……………………………………………………………………………………...
2. Stool …………………………………………………………………………………...
3. T.B. Test ……………………………………………………………………………….
4. Syphilis Test ……………………………………………………………………………...
5. Urine Examination ………………………………………………………………………….
6. Eye Test ……………………………………………………………………………….
7. Chest Test ……………………………………………………………………………...
8. Ears Test ……………………………………………………………………………….
9. Spleen ………………………………………………………………………………….
10. Abdomen ………………………………………………………………………………
11. Pregnancy………………………………………………………………………………

ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment, infection, family diseases etc.
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

I certify that, the above pupil is suitable/unsuitable for secondary school students. If unsuitable give reasons:
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

Name of Medical Officer: …………………………………………… Signature ………………………

Date: ……………………………………… Official stamp ………………………………

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

FOMU NAMBA 2.

TAARIFA ZA ANAKOTOKA MWANAFUNZI

1. Mkoa ………………..……………………… Wilaya …………………………………………
2. Tarafa ……………………………………………. Kata ………………………………………
3. Mtaa/Kijiji ……………………………………………
4. Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………..………….Saini………………….
   Tarehe……………………………… Mhuri……………………………. Simu…………………...
5. Michezo anayopendelea

| Na. | Jina la Mchezo |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |
| 4. | |
| 5. | |

9. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| Na. | Aina ya uongozi | Shule | Mwaka |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo.

NB: Pamoja na fomu hizi ambatanisha na kopi ya cheti cha kuzaliwa na nakala halisi ya matokeo.

Jina la Mwanafunzi ……………………………………..Saini ………………… Tarehe ……………

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

---

FOMU NAMBA 3.

TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………….
2. Kazi ……………..…………………………………………………………………………………...
3. Anuani ………………………………………… Namba ya simu ……………………………….
4. Mkoa ………………………… Wilaya ……………………….. Tarafa ………….………………
5. Kata ………………………………………Mtaa/Kijiji ……………………………………………

6. Ndugu wa karibu wa mwanafunzi

| Na. | JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………… ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari Ilulu katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya.

Jina la Mzazi/Mlezi ……………………………………Saini …………………Tarehe ………………..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

GENERAL STUDIES

1. Understanding General Studies for advanced level. JOANNES BIGIRWAMUNGU
2. General Studies alive – ZISTI KAMILI

HISTORY 1

1. Personal supplier madaya himself

HISTORY 2

1. Contemporary historical events – volume 2 by shibitali C. K
2. Essentia ls in Advanced level Histor y – book 2 by saleh yassin
3. Mast ering Advanced level Histor y – book 2 by Abubakar kato
4. Advanced level history – part two alive by Zisti Kamili

KISWAHILI 1

1.Kiswahili 1 kidato cha 5 na 6 (TIE)
2. Nadharia ya lugha - Nyambari na Masebo

KISWAHILI 2

1. Nadharia ya fasihi Kiswahili 2 kidato cha 5 na 6
2. Kiswahili 2 (Tahakiki ya Kiswahili) shule za sekondari, kidato cha 5 na 6.

ENGLISH 1

1. Nicholaus Asheri: Advanced level English
2. Francis Mnyawi: Contemporary English for Advanced level
3. Kadeghe Michael: Advanced level English form 5
4. Oxford Advanced level English form 5 & 6

ENGLISH 2

1. Nicholaus Asheri: Advanced level English Literature
2. Nyambari Nyangwine: Advanced level English Literature
3. Francis Mnyawi: Advanced level English Literature

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI
SIMU: 0782586468/0717402768
0688800033/0713118885

SHULE YA SEKONDARI ILULU
S.L.P 139, KILWA.
ilulugss@gmail.com

GEOGRAPHY 1
1. Physical geography – Zisto Kamili (2016
2. Physical geography integrated Approach – by David Waugh

GEOGRAPHY 2
1. HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY PAPER 2 BY MSABILA DT

CHEMISTRY 1
1.Conceptual Chemistry for class xi: Dr. S.K Jain
(CHAND ONE)
2. Hopegen book project (HBP) Physical chemistry (NGAIZA SERIES)

CHEMISTRY 2
1. Hopegen book project (HBP) (ORGANIC CHEMISTRY (NGAIZA, LUSIMA
2. Chemistry for secondary school form five (TIE)

BAM
1. Basic Applied Mathematics for Advanced level secondary schools: By Tanzania Institute of Education (T.I.E), (2019)

BIOLOGY 1
1. Biology foe advanced level secondary school
2. Student’s book form five – Tanzania institute of education (TIE, 2019)
3. Dissecting kit

BIOLOGY 2
1. Biology foe advanced level secondary school
2. Student’s book form five – Tanzania institute of education (TIE, 2019)

